

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
3 Barabara ya Rashidi Kawawa,
S.L.P 5429,
12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mheshimiwa Paul C. Makonda Leo 18 Mei, 2017 amezungumza na Watendaji wa Sekta ya Ardhi na Ujenzi wanaohudumu katika Manispaa za Ubungo, Kigamboni, Kinondoni, Temeke, Ilala na Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ambapo ametoa maelekezo 17 ya kuzingatia katika utendaji wao.

1. Watendaji wa Sekta ya Ardhi na Ujenzi Kushughulikia migogoro ya Ardhi na Ujenzi ili wananchi wasipeleke malalamiko yao ngazi za juu.
2. Watendaji wa Sekta ya Ardhi na Ujenzi Wameagizwa kutoa vibali vya Ujenzi ndani ya mwezi mmoja na zoezi hilo lianze mwezi wa sita mwaka huu 2017. Mwanzoni mwa mwezi wa Saba kuzinduliwa teknolojia ambayo wananchi watapata taarifa zao za Ardhi kwenye mtandao jambo ambalo litafanya Dar es salaam kuwa kiganjani mwa wananchi.
3. Wakuu wa Idara katika Sekta ya Ardhi na Ujenzi kuhakikisha wanatoa taarifa kuhusu Mipango ya Idara kwenye vyombo vya habari kwa kuwatumia maafisa habari kwani tayari wana mahusiano na waandishi mbalimbali katika vyombo vyombo vya habari.
4. Wakuu wa Idara ya Ardhi na Ujenzi kutoa **TAARIFA** ya maeneo yote ya wazi yaliyotolewa Hati, na kujitokeza haraka kwa wote waliotoa Hati za maeneo ya wazi kama wapo.
5. Wakuu wa Idara ya Ardhi Na Ujenzi kusimamia haraka upimaji wa maeneo yote ya Umma kama kama vile Shule, Hospitali, na Masoko kama alivyoagiza Waziri wa TAMISEMI sambamba na kutoa Mikakati ya Upimaji.
6. Wakuu wa Idara ya Ardhi na Ujenzi kuhakikisha ufanisi na bidii ya utendaji inaongezeka hususani mikakati ya kuhusisha wapimaji binafsi wanaotambulika kwani Mji ukipimwa vyema Madiwani watafurahi lakini pia itakuwa njia rahisi ya kuepuka migogoro ya Ardhi.

7. Kushughulikia changamoto za kisera zinazofanya utaratibu wa Upimaji na utoaji wa Hati kuchelewa kukamilka.
8. Mabaraza ya Kata kuangaliwa upya kwa mujibu wa Sheria ili kuwa na utendaji imara unaoshabihiana na jambo la kisera.
9. Kila Mtumishi kufanya kazi yake kwa Uaminifu kwani dhamana aliyopewa ni kubwa na anapaswa kuitendea Haki. Watumishi wote kusimamia na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwani chama hicho ndicho kimeingia mkataba na wananchi katika kipindi cha miaka mitano.
10. Kila Mkuu wa Idara kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015 - 2020 ili kutambua maelekezo yaliyobainishwa katika Sekta yake sambamba na kuwaelekeza wasaidizi wao pia kuisoma na kuielewa vyema Ilani hiyo.
11. Kufatilia na kufahamu upandaji wa madaraja na stahiki zao kwani ni Haki zao za msingi kisheria ikiwa ni pamoja na kwenda likizo.
12. Watumishi wote kuheshimu mamlaka walizonazo na kutumia vikao halali kutoa taarifa sahihi kwa watu husika.
13. Kuwa na ushirikiano wa watumishi katika Idara zote ili kukuza ufanisi wa Kazi.
14. Kujitokeza ndani ya wiki moja kwa watumishi wote wa Sekta ya Ardhi waliojijhusisha na utoaji wa Hati za Ardhi kinyume na sheria na endapo wasipojitokeza na wakabainika watachukuliwa hatua za kisheria.
15. Kufafanua baadhi ya mambo ili Madiwani waweze kuelewa sambamba na kutoogopa maadhimio kama wanatenda kazi kwa mujibu wa Sheria pasipo kupendelea.
16. Wakuu wa Idara kila mwisho wa wiki kutoa taarifa kwa Wakurugenzi inayoonyesha idadi ya Migogoro na jinsi ilivyotatuliwa.
17. Katika kupunguza changamoto ya kuwafikia wananchi kwa Wakati Mkuu wa Mkoa amesema atatoa Pikipiki 5 kwa kila manispaa ya jiji la Dar es salaam, yaani jumla ya pikipiki 25 kwa manispaa zote 5 za Sekta ya Ardhi kwa kila Manispaa.

Imetolewa Na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano
OFISI YA MKUU WA MKOA
DAR ES SALAAM
18/05/2017